**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

# MUONGOZO WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA JAMII (ESMF)

## MRADI WA KUBORESHA MILKI YA ARDHI

**(Land Tenure Improvement Project)**

**Februari 2020**
**DODOMA**

## MUHTASARI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inaandaa mradi wa kuboresha milki ya ardhi nchini. Mradi huu unalenga kuongeza usalama wa haki za ardhi na ufanisi kwenye utawala wa ardhi katika maeneo ya ya Mijini na Vijijini na hivyo kukuza uwekezaji na pato la Taifa. Maeneo ya kiutekelezaji ya mradi yatakuwa ni (1) kuongeza usalama wa milki za Ardhi kwa kupanga, kupima na kumilikisha Wananchi Ardhi Mijini na Vijijini (2) kuboresha mifumo ya usimamizi wa taarifa za ardhi nchini (3) kuimarisha uwezo wa Wizara na taasisi zake na ( 4) usimamizi na ufuatiliaji wa mradi. Mwongozo huu umetayarishwa kwa kuzingatia mahitaji na maelekezo ya Benki ya Dunia ya kulinda haki ya mazingira na jamii. Pia umezingatia sheria, sera, kanuni na taratibu za ardhi, mazingira na ujenzi nchini.

Mradi huu ni mwendelezo wa miradi ya aina hii ambayo imetekelezwa nchini ndani ya muongo mmoja uliyopita. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa maboresho ya milki za ardhi katika Mkoa wa Morogoro, Usajili na utoaji hati katika Mkoa wa Iringa, mradi wa maboresho ya makazi katika jiji la Dar Es Salaam na Mwanza, na Mradi wa viwanja 20,000 katika jiji la Dar Es Salaam.

Viashiria vya matokeo yanayotarajiwa katika Mradi huu ni pamoja na: idadi ya hati milki, Idadi ya hati milki za kimila, idadi ya leseni za makazi zilizotolewa na kusajiliwa vyote kwa kuzingatia jinsia; ongezeko la miamala ya ardhi, kupungua kwa migogoro ya ardhi, kuongezeka kwa usalama wa milki kwa kuzingatia haki na jinsia. Kimsingi utekelezaji wa mradi utahusisha Mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini. Utekelezaji wa Mradi huu utagharimu kiasi cha dola za kimarekani milioni mia moja na hamsini.

Katika eneo la kuongeza usalama wa milki za Ardhi, mradi utalenga kutekeleza shughuli zifuatazo: Kutoa kwa wingi hati milki na leseni za makazi katika maeneo mijini; na kutoa hati milki za kimila za ardhi kwa wingi katika maeneo ya Vijiji. Miongoni mwa shughuli nyingine, eneo hili litasaidia kukuza uelewa na kuimarisha mfumo wa usimamizi wa haki za ardhi kwa kuzingatia kanuni za Mazingira na Jamii za Benki ya Dunia vifungu nambari 5 na 10 (ESS 5 na ESS10).

Katika kuboresha mfumo wa usimamizi wa taarifa za ardhi nchini, shughuli zitakazofanywa katika eneo hili ni uboreshaji na usambazaji wa mfumo unganishi wa taarifa za ardhi (ILMIS) katika Mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini, maboresho ya mtandao wa jiodesia, upigaji wa picha za anga, uchoraji wa ramani za msingi, na kuanzishwa kwa miundombinu ya utunzaji wa kumbukumbu za kijiografia). Miundo mbinu hii itasaidi upangaji na upimaji wa ardhi, na pia kujenga kanzidata ya taarifa za ardhi kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya ardhi nchini. Eneo hili pia litajumuisha ujenzi wa ofisi 26 za Ardhi za Mikoa, kuweka miundo mbinu unganishi katika ofisi hizi, ununuzi na ufungaji wa vifaa katika ofisi za ardhi za Mikoa zitakazojengwa. Athari za kimazingira na kijamii zinaweza kujitokeza katika jamii zinazozunguka maeneo ya ujenzi kutokana na

uzalishaji taka, matumizi ya malighafi na ongezeko la wafanyakazi katika shughuli za ujenzi.

*Katika kuimarisha uwezo wa Wizara na taasisi zake*, shughuli zitakazofanyika ni pamoja na maboresho ya sera, sheria na kanuni za ardhi, kuwajengea uwezo wa watumishi wa sekta ya ardhi, kuelimisha umma kuhusiana na masuala ya ardhi na kuboresha utoaji wa huduma za ardhi, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa. Shughuli nyingine zitakazitekelezwa zitajumuisha kujenga uwezo kwa watekelezaji wa mradi, wamiliki wa ardhi mijini na vijijini na kuimarisha shughuli zingine za sekta mtambuka katika kuwezesha usimamizi, uendeshaji na uratibu wa mradi.

*Katika usimamizi na ufuatiliaji wa mradi*, eneo hili linalenga kuhakikisha mradi unatekelezwa kwa uhakika na kwa ufanisi ili kupata matokeo sahihi yanayoendana na thamani ya fedha iliyotumika. Eneo hili litajumuisha shughuli mbalimbali zikiwemo ukusanyaji na uhakiki wa taarifa za awali za hali halisi kwenye maeneo ya mradi, usimamizi wa utekelezaji wa nyaraka za miongozo ya kimazingira na kijami, ufuatiliaji wa shughuli katika maeneo ya mradi, usimamizi wa kaguzi mbalimbali za mradi, kuunda mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa mradi, kusimamia haki za wafanyakazi, kuandaa taarifa za robo mwaka na za mwaka za mradi na kufanya tathmini za mwisho za matokeo ya mradi.

Utekelezaji wa Mradi huu utazingatia kanuni za kimazingira na kijamii za Benki ya Dunia. Kulingana na kanuni, mradi umeanishwa kuwa na hatari ya kiasi hususani kutokana na taratibu za umilikishaji wa ardhi, shughuli za ujenzi, maeneo ya mradi, unyeti wa zoezi, kiwango cha kazi, asili ya mradi na uwezo wa Taasisi inayotekeleza. Shughuli hizi zitapimwa kulingana na matakwa na mahitaji ya kanuni za kimazingira na kijamii za Benki ya Dunia. Vile vile kutakuwa na uhuhishaji wa mara kwa mara wa utekelezaji wa kanuni hizi ili kuondokana na athari za kimazingira na kijamii. Mpango wa uwajibikaji wa kimazingira na kijamii (ESCP) umeandaliwa na umeweka vipimo ambavyo mradi utapaswa kufikia wakati wa utekelezaji.

Sambamba na kanuni za kimazingira na kijamii za Benki ya Dunia, mradi utazingatia sheria za nchi katika kuhifadhi na kulinda mazingira, maliasili, urithi wa kitamaduni huku ukihakikisha usalama na afya za washiriki katika mahali pa kazi. Kwa kumbukumbu, sheria za msingi zitakazotumika ni pamoja na sheria ya usimamizi wa mazingira (EMA) (2004), sheria ya ardhi ya Vijiji nambari 5 (1999), sheria ya ardhi ya nambari 4 (1999) na Sera ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2002. Sera na sheria zingine ni pamoaja na Sheria ya afya na usalama wa kazi nambari 5 ya 2003, sheria ya ajira na uhusiano nambari 6 ya 2004, sheria ya upangaji wa miji ya mwaka 2007, Kanuni za tathmini ya athari ya mazingira na ukaguzi ya mwaka 2005, sera ya Taifa ya ardhi ya mwaka (1995), sera ya jinsia (2011), sera ya maendeleo ya kilimo na mifugo (1997), sera ya misitu ya Taifa ya mwaka 1998, sera ya mazingira ya kitaifa ya mwaka 1997, sera ya Taifa juu ya VVU/UKIMWI ya mwaka 2001, sheria ya afya ya jamii ya mwaka 2001, sheria ya trafiki ya barabarani ya mwaka 2002 iliyorejewa mwaka 2018 na sheria ya afya ya umma ya mwaka 2012. Vilevile, sera, sheria na mipango ya kisekta zitazingatiwa katika kushughulikia masuala ya kijamii na kimazingira katika utekelezaji wa shughuli za mradi.

Utekelezaji wa mradi huu utazingatia kanuni za kimazingira na kijamii ili kuepuka matokeo mabaya yoyote ya utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa na hivyo kuimarisha na kuboresha viwango vya maisha kwa watu maskini Vijijini na Mijini. Athari hasi za kimazingira na kijamii zinazotarajiwa katika shughuli za umilikishaji ardhi ni pamoja na upotevu wa haki ya ardhi ambayo inaweza kusababisha mtu kupata hasara za kiuchumi, hatari za kuongezeka unyanyasaji wa kijinsia kutokana na uwepo wa timu za utekelezaji, kuongezeka kwa maambikizi ya magonjwa ikiwa ni pamoja na UKIMWI kutokana na mwingiliano na jamii, migogoro ya ardhi inayotokana na ushindani wa haki za ardhi kati ya Wakulima na Wafugaji, mwingiliano wa madai kwenye kipande kimoja cha ardhi na upotevu wa haki nyingine za ardhi zaidi ya zile za mmiliki ikiwemo ile ya upangaji, njia, mkopeshaji n.k. Kuna hatari pia ya kuwatenga makundi maalumu kwa mfano wanawake, walemavu, wazee ambao hawajapata taarifa za mradi kutokana na hali zao na kutokuwa na usawa katika kutoa haki za ardhi kwa sababu ya mifumo dume ambapo wanaume wanafanya maamuzi juu ya masuala ya ardhi. Athari za kimazingira zitaepukika kutokana na zoezi la uchaguzi na uhakiki wa maeneo ya mradi ili kuepuka kutoa hati kwenye maeneo ya hifadhi, hatarishi na njia za Wanyama pori.

Inatarajiwa kwamba shughuli za urasimishaji zitakuwa na athari ndogo and kutokuwa na athari kwani hazitahusisha shughuli za moja kwa moja ukiacha ile ya kuweka vigingi kwenye maeneo ya umma. Wakati wa ujenzi wa majengo ya ofisi, athari za kimazingira zitajumuisha usafishaji wa viwanja, mmomonyoko wa udongo na vumbi kutokana na uchimbaji ardhi, uchafuzi wa mazingira, hewa na maji vinavyosababishwa na taka za ujenzi. Athari za kijamii zinazotokana na ujenzi zitajumuisha uhamisho wa watumiaji wa ardhi toka maeneo yao ya asili, kuongezeka kwa maambukizi ya magonjwa na unyanyasaji wa kijinsia utakaotokana na ongezeko la wafanyakazi na hatari za ajali za barabarani. Majengo pia yatahitaji kuwa imara ili kupunguza hatari yoyote kwa afya na usalama wa jamii. Kwa nyongeza, katika maeneo yote ya mradi, kazi na hali za kazi za wafanyakazi ikiwa ni pamoja na afya na usalama wa mahali pale vitahitaji kusimamiwa.

Hatua za kukabiliana na athari zilizoelezwa hapo juu ni pamoja na: kuhimiza makampuni kutumia wafanyakazi na vibarua kutoka ndani ya eneo la mradi pale inapowezekana ili kupunguza idadi ya wafanyakazi kutoka nje ya eneo la mradi, washauri na makandarasi waandae miongozo ya utendaji wa wafanyakazi kama sehemu ya mikataba ya ajira, kuwaongezea uelewa kwa wafanyakazi na wadau juu ya VVU/UKIMWI ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi ya kondomu, hatua za kujizuia na kujikinga, kuhudumia mgonjwa, kutoa ushauri nasaha na kupima, kukuza uelewa kwa wafanyakazi na wadau juu ya unyanyasaji wa kijinsia, ukosefu wa usawa wa kijinsia, mpango wa usawa wa kijinsia, wanawake kuhimizwa kushiriki katika kazi za ujenzi. Baadhi ya kazi zinaweza kutolewa kwa wanawake ili kuhamasisha ushiriki wao na kuboresha mapato yao. Kampuni binafsi na washauri kuanzisha mbinu za ukaguzi na uchujaji ili kuhakiki umri na kutambia hali za wafanyakazi wakati wa ajira, utoaji wa vifaa vya kufanyia kazi, makandarasi kufanya mikutano ya kazi kuwakumbusha wafanyakazi juu ya masuala ya afya na usalama kazini. Pia maeneo yote ya mradi ya ujenzi kusajiliwa na OSHA kwa mujibu wa sheria ya afya ya kazi na usalama wa mwaka 2003, ardhi itakayotolewa na mmilki kwa matumizi ya umma haipaswi kuzidi asilimia 5. Endapo itazidi asilimia 5, taratibu za kulipa fidia zitafuatwa

kulingana na sheria za nchi na kanuni za Kimazingira na Jamii za Benki ya Dunia, utoaji wa ardhi mbadala kwa ajili ya mradi inapaswa pia kuzingatiwa pale ambapo fidia haiwezekani, kuweka utaratibu wa utatuzi wa migogoro kwa wafanyakazi kuwasilisha malalamiko na madai yao, ukaguzi wa mara kwa mara wa mikataba ya ajira, kazi na mazingia ya utendaji kazi kwa makandarasi na makampuni ya binafsi, utoaji wa hati milki za Kimila za pamoja kwa ajili ya maeneo yenye raslimali zote za pamoja, uanzishwaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na uhamasishaji wa jamii juu ya haki za ardhi, makandarasi kuhakikisha ukusanyaji sahihi wa taka, uhifadhi na usimamizi wa taka, makandarasi kuepuka kumwaga mafuta ovyo kwa kutumia vyombo wakati wa matengenezo na makandarasi kuhakikisha kwamba malori yanafanyiwa matengenezo ya mara kwa mara ili kupunguza usambazaji wa hewa chafu.

Mpango wa usimamizi wa kanuni za Kimazingira na Kijamii wa mradi umeandaliwa kushughulikia athari yoyote itakayojitokeza. Michakato ya urasimishaji itatoa hati milki na hati milki za kimila. Nyaraka hizi haziruhusiwi kisheria kutolewa kwenye maeneo yaliyohifadhiwa, au maeneo ya viumbehai, njia za wanyamapori, maeneo uevu na mengine nyeti kimazingira. Mradi unatarajiwa kutoa hati milki 1,000,000, leseni za makazi 1,000,000 na hati za haki milki zipatazo 500,000. Nyanda zote za malisho zitafuatiliwa ili kuhakikisha kwamba jamii za wafugaji wanajumuishwa katika mipango yote ya upangaji na maamuzi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi. Zaidi ya hayo, mradi huo hautaanza kutoa hati milki za kimila kwenye maeneo ya Arusha isipokuwa katika maeneo ambayo kuna migogoro michache baina ya Wakulima na Wafugaji ili Wizara na Timu za utekelezaji zijenge uzoefu. Wakati wa utekelezaji wa mradi Mkoani Arusha, kutakuwa na uzoefu wa kutosha wa timu za utekelezaji na hivyo utahakikisha umehusisha na kujumuisha asasi za kijamii na kiraia zenye uzoefu wa kushughulikia masuala ya wafugaji. Hii itasaidia kutatua migongano inayoweza kujitokeza na hivyo kutosababisha migogoro. Uhakiki wa maeneo ambayo hati milki na hati milki za kimila zitotolewa utafanyika hatua kwa hatua ili kuhakikisha kwamba athari yoyote itakayoweza kujitokeza inatambuliwa mapema na njia sahihi za utatuzi kuwekwa kabla ya kuanza kwa mradi katika eneo hilo.

Katika uhakiki wa hali halisi ya maeneo ya mradi, Kitengo cha uratibu wa utekelezaji wa mradi kwa kushauriana na kushirikiana na taasisi nyingine za kiserikali zinazohusiana na Wanyamapori, Hifadhi za taifa, rasilimali za maji na maeneo yaliyohifadhiwa yatatathmini athari za kijamii na kimazingira zitakazosababishwa na urasimishaji na kazi za ujenzi katika hatua za utekelezaji wa mradi kwa kutumia nyenzo ya uhakiki iliyoandaliwa na kuwekwa kwenye mwongozo huu. Hii itasaidia kuonesha kama matokeo hasi au chanya ya kimazingira na kijamii yatatokea wna hatua za kukabiliana nazo kuandaliwa baada ya kutambuliwa. Vile vile, kitengo kitahaki athari za kimazingira na kijamii katika maeneo ya ujenzi. Aina ya nyenzo ya uhakiki na tathimi zitafuata kanuni za kimazingira na kijamii kwa mujibu wa Sheia ya Mazingira ya nchi ya mwaka, 2004, Kanuni za tathmini na athari za Kimazingira na marekebisho yake ya mwaka 2018, pamoja na kanuni za kimazingira na Kijamii za Benki ya Dunia (ESS1, ESS2, ESS5 na ESS10).

Utekelezaji wa urasimishaji wa ardhi na ujenzi wa majengo ya Ofisi za ardhi za Mikoa utahusisha ajira ya muda katika maeneo ya mradi. Katika hali hii, taratibu za usimamizi wa wafanyakazi zimeelezewa katika mwongozo huu ili kukidhi malengo ya Kanuni na

Mahitaji ya Benki ya Dunia (ESS 2 na ESS4) kwa ajili ya kuhakikisha afya na usalama mahala pa kazi. Taratibu za usimamizi za wafanyakazi zinatoa mahitaji ya usalama, matumizi ya vifaa vya kinga binafsi na utayari wa dharura ukiwa kazini. Mradi utatumia mahitaji husika ya afya ya mazingira na miongozo ya usalama

Mwongozo wa usimamizi wa Mashirikiano na Wadau umeandaliwa kama nyaraka ya kipekee kwa mujibu wa mahitaji ya Benki ya Dunia (ESS10). Hii itahakikisha kuwa wadau wote wa mradi wameshirikishwa kikamilifu katika hatua zote za shughuli za mradi kama zinavyoonekana pia katika za Mashirikiano na Wadau na Uhamishaji Makazi. Vile vile, mradi huu utaanzisha utaratibu wa kushughulikia malalamiko ili kuhakikisha kwamba yanasikilizwa na kutatuliwa. Mpango wa uhamasishaji na uwezeshaji wa wadau katika kutekeleza kanuni za kimazingira na kijamii na bajeti vimejumuishwa katika mwongozo wa usimamizi wa Kimazingira na Kijamii ambayo itakuwa ni kipaumbele cha kwanza kabla ya ya utekelezaji halisi wa shughuli za mradi katika maeneo ya mradi nchini.

**HUU NI MUHTASARI TU WA MUONGOZO WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA JAMII**

ANDIKO ZIMA LINAPATIKANA KUPITIA:-
**Tovuti: www.lands.go.tz**

KWA MAONI NA USHAURI TUMA KUPITIA:-

**Barua pepe:** wakuru.maseka@lands.go.tz, lucy.kabyemera@lands.go.tz, Mariam.silim@lands.go.tz

**Simu/ Ujumbe wa simu: +255767322277, +255713278040, 0683214181**

Anwani: **Katibu Mkuu**
Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.
S.L.P 2908.
**Dodoma.**